



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI MBEYA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MCC/E.40/6/VOL. III/13

14/04/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya amepata kibali cha ajira mbadala cha tarehe **15 Machi, 2022** chenye **Kumb.Na.FA. 170/364/01 "B"/29** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Hivyo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenyewe sifa zinazotakiwa kujaza nafasi ifuatayo:-

1 DEREVA DARAJA II – NAFASI (7)

1.1 SIFA ZA MWOMBADI

Waombaji wawe na cheti cha kidato cha Nne (form IV) na leseni ya daraja la E au C.1 ya uendeshaji wa magari ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka (1) bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambulika na Serikali. Waombaji wenyewe cheti cha majaribio ya ufundu Daraja la II watafikiriwa kwanza.

1.2 MAJUKUMU

- i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- v) Kujaza na kutunza taariza za safari zote katika daftari la safari,
- vi) Kufanya usafi wa gari na,
- vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyo elekezwa na msimamizi wake wa kazi.

1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya serikali yaani TGS B.

2. MASHARTI YA JUMLA

- i) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
- ii) Waombaji wawasilishe picha mbili za hivi karibuni.
- iii) Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenyne anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- iv) Waombaji waambatanishe nakala ya vyeti vya masomo na taaluma na cheti cha kuzaliwa. Muombaji atakayewasilisha "Result slip" "Statement of results" "Provisional results" au "Transcript". **HAVITAKUBALIKA.**
- v) Kwa waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitahani la Tanzania (NECTA).
- vi) Kwa waliomaliza vyuo nje ya nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).
- vii) Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika usaili.
- viii) Waombaji waandike namba ya kitambulisho cha Taifa katika barua za maombi au waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- ix) **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 28/04/2022 saa 9:30 Alasiri.**

MUHIMU: Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na nyaraka zote zinazohitajika. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji la Mbeya,
S.L.P 149,
MBEYA.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.mbeyacc.go.tz.

Tangazo hili limetolewa na:-


Triphonia A. Kisiga
**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA.**

*MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA*